***Ministère de la Santé Publique***

***Secrétariat Général***

*Direction Nationale de l'Hygiène*

# VILLAGE ASSAINI

## ALBUM A FEUILLETS EN SWAHILI

Réalisé par l'Equipe Nationale des Formateurs en Eau et Assainissement (**ENFEA**)
en collaboration avec l'UNICEF pour le Programme National « **Village Assaini** »

**2011**

**VITOKEZO KWA WATUMIYAJI**

Buku hii ina Vipindikenda (9) zenye kuhusika na jamaa za vijijini pamoja na hizo zenye kuishi kandonkando ya miji mikuu ya Jamuhuri ya kidemokrasia ya Congo, Katika niya ya kuboresha Usafi ya wakaaji binafsi na piya mazingira zao kupitiya muradi ya serekali "Village assaini"

Vipindi Hivyo Vimepangwa namna ifwatayo

1. Matumizi ya maji safi yatokayo mahali zilizo kuwa safi
2. Namna ya kuweka na kuchunga maji safi nyumbani
3. Kuosha mikono Kiishaya kutumiya choo/Musirani (WC)
4. Kuosha mikono mbele ya kula
5. Utumiyaji ya choo safi
6. Usafi ya mapango
7. Kuondowa vema ushafu wa nyumbani
8. Kazi mbalimbali ya vikundi vijijini kuhusu usafi
9. Kuhimarisha kazi za mradi kwa msaada ya kamati ya vijiji

Mabamba hizi zina hesabiwa kutoka 1 mpaka 9, zime wekwa mapicha upande ya kwanza, kiisha maswali na majubu, na piya matangazo mbalimbali upande ya pili.

Mutumiyaji ya Album hii ni mtu yoyote anaye tambuliwa na Mganga mkuu wa kituo cha afia kuwa kama vile Muhimizaji mkuu wa makundi mbalimbali, ao musimamizi wa kazi kuhusu maji na usafi wa mazingira. Hivyo, mtu yoyote ambaye anaweza kusoma, na ambaye amepata majifunzo ya kutosha anaweza kujaribu kutumiya album hii. Hawa watumiyaji wenye kujitowa kwa Utashi yao inawezekana wawe kwa mfano wanamemba wa relais communautaires (RECO), wajumbe wa makundi ya dini, waelimushaji, na watu wenye kuheshimika katika mji (Leaders communautaires).

Album hii siyo chombo chenye kuboresha mahusiyano peke yake, ila ina ongeza zaidi bahati za mikutano na mazungumuzo kwa manufaa ya kubadili tabiya.

Namna ya kutumiya album hii imepangwa ifwatavyo:

- Mutumiyaji ya album anaweza ongoza mazungumuzo na jamaa tatu kwa siku moja. Inahitaji, kama kidogo siku 7 ili aweze kuzunguka jamaa makumi mawili (20)
- Vikaratasi vya album hii vinapashwa kutumiwa tangu namba ya kwanza, mpaka ya mwisho.
- Inafaa dakika makumi tatu (30min) kwa mukutano mmoja.
- Mutumiyaji ya album hii anaweza kutembeleya zaidi ya mara moja ndani ya jama moja

Katika ngazi ya jamaa

- Tumiya maswali na majubi kwa kuongoza mazungumuzo;
- Omba wanamemba wa jama watambuwe pekee yaho uhusiyano kati ya maandiko na mapicha
- Tambuwa, pamoja na wanamemba wa jama sababu gani zinaweza kuzuiya ku shika tabiya mpya, kiisha ufikiriye pamoja nawo, suluhisho kwa kizuwizi hicho.
- Himiza wanamemba ya makundi mbalimbali ili wafikiye kushika tabiya mpya, kiisha mupangilye siku ijayo ju kufwatiliya mambo hayo.

**NDANI YA VIJIJI VWETU, MARA NAMARA TUKUNYWE MAJI SAFI KUTOKA MAHALI ILIYO SAFI NA YENYE UKINGO BORA**

**ULIZO 1: MUMEONA NINI KWENYE PICHA HII?**

**JIBU 1**: Watu watatu: Mama moja ana jerekani ya litre 10 kwenye mkono wake wa kuume, anangojeya mbeketi ijae maji kutoka kisima kilicho jengwa. Musichana momoja amekuisha shota maji kati ya Mbeketi na jerkani ya litre tano. Mtoto kijana anabeba jerekani ya litre tano kwamukono wa kuume, naye anangojeya wakati yake ya kushota ifike ili aweze shota.

**ULIZO 2: NI WAPI NDIYO MAHALI KAMILI YAKU TAFUTIYA MAJI NDANI YA KIJIJI CHENU?**

**JIBU 2**: Sikiliza majibu: Mujibu kama mahali vema ni kwenye Robinet, Bomba, visima vya maji ya kitiririka vyenyi kujengwa, visima vyenyie kujengwa dani ya udongo.

**ULIZO 3: KWA NINI INAFAA KUYWA MAJI TOKA KWENYE VISIMA VYENYE KUJENGWA?**

**JIBU 3**: Ili tu epuke magonjwa inayo tokeya kwa utumizi ya maji machafu, kama vile kuharisha, kipindupindu, Tifoide, Kuharisha damu, Virisu vya vunjavunja nayo piya nanaletwa na maji machafu.

**HABARI ZINGINE**

- Kama hakuna maji kutoka mahali safi, inatuomba kutokosha maji. Maji yenye kutokosha mpaka degri miya moja hu kamata Oxygene na onjo yake ya kawaida. Ila ni vema zaidi kunywa maji isiyo na onjo ila isiwe na vidudu.
- Tunapashwa kushota maji ndani ya chombo safi. Kuisukuwa vizuri mbele ya kushota
- Kufunika vizuri chombo chakushoteya maji ili tukinge maji na vidudu wakati ya kubeba maji toka kisima mpaka nyumbani
- NDani ya nyumba, funika vizuri chombo cha kuweka maji, mahali palipo inuka juu, nafasi isiyo fika watoto na manyama za nyumbani
- Weka kandokando ya chombo ya kuweka maji, chombo kingine chaku shota maji, ila isiwe jerekani wala mbilika
- Shika vema kuwapatiya maji ya kunywa watoto wote wa umri ya chini ya mwaka tano ju tukinge vema chombo cha kuweka maji zidi ya uchafu mbalimbali



**TUCHUNGE MAJI SAFI YETU  KILA MARA NDANI YA VYOMBO VILIVYO SAFI**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA  NINI   KWENYE  PICHA  HII?**

**JIBU 1**: Picha ya mama anaye shota maji toka jerekani ya 5 litres aki kutumiya kopo. Juu ya meza, kuna jerikani ya 10 litres, 20 litres. Mutungi inayo kuwa na kifuniko, na bakuli ya rangi nyekundu. Mutoto mumoja  msichana anakunywa maji  kwa akitumia kopo, mwengeni anagojeya kupewa maji.

**ULIZO 2: KWA NINI NI LAZIMA KUWAPATIYA WATOTO KIDOGO MAJI SAFI?**

**JIBU 2**: Juu maji iliyo safi haina vidudu vyenye kuleta magonjwa

**ULIZO 3: KWA NINI WATOTO WADOGO HAWAPASHWE  KAMATA MAJI  SAFI PEKE YAO?**

**JIBU 3**: Watoto kidogo wanaweza chafuwa maji  ipatikanao ndani ya vyombo vyakuweka maji nyumabani.

**ULIZO 4: SABABU GANI MAMA WA JAMAA ANAPASHWA  KULINDA MAJI SAFI  NDANI YA CHOMBO KINACHO  FUNIKWA?**

**JIBU 4**: Ni ju ya kuzuwiya uchafu, vumbi na vidudu vibaya visi ingiye ndani ya chombo chakuweka maji

**ULIZO 5: NYUMBANI KWENU, NI NAFASI GANI NA NAMNA GANI MUNACHUNGA MAJI  YA KUNYWA?**

**JIBU5**: Mushike vema majibu na pia muongezeye  na habari  zifwatayo:

- Kuchunga vyombo vyakuweka maji nafasi iliyo inuka  juu
- Kuchunga vyombo vya maji mbali na watototo wadogo
- Kutafautisha vyombo vya kuchukuwa maji umbalimbali na vile vya kuywa
- Kufunika vizuri vyombo vya kuchunga maji
- Kunywa peke yake maji kutoka visima vilivyoa jengwa
- Epuka kunywa maji kutoja mtoni wala Bahari ama Visiwa



**Tunawe mikono na sabuni ao majivu kiisha kutoka kwenye choo.**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI KWENYE PICHA HII?**

JIBU1: Wabwana wawili, mumoja ana mimiya maji kwa mikono ya mwenziye kwa kutumiya kopo, choo (WC), Nyumba, na sabuni juu ya kiti fupi.

**ULIZO2: HAYO MAMBO YOTE, INA FUNDISHA NINI?**

JIBU2: Kunawa mikono na sabuni kiisha choo kubwa

**ULIZO 3: KUNA NAMNA INGINE YA KUNAWA MIKONO?**

JIBU3: Ndiyo, kunawa mikono kwa kutumiya chombo iliyo tengenezwa na myanzi, ao kutumiya jerekani ndogo ndogo;

**ULIZO 4: SABABU GANI TU NA PASHWA KUNAWA MIKONO KIISHA CHOO?**

JIBU4: Sababu ni ukingo wa ngufu saana kwa kuzuwiya vidudu ku fika ndani ya kinywa kupitiya mikono ya mtu. Mavi ni njiya halali ya mangonjwa iitwoya, ya uchafu, zaidi, Kipindupindu, na Tifoide.

**Habari zigine**

- Inakatazwa kunawa mikono katika vyombo vya kuweka maji, ni lazima maji itiririke kwa mikono
- Tuta weza piya kujenga chombo cha kunawa mikono kwa kutumiya:
    - Mbeketi ya plastike
    - Kipande ya Mwanzi
    - Mbilika
    - Chombo chochote Kilicho tumiwa ama Jerekani
    - Vile vile, ni lazima kwa wazazi kunawa mikono yao baada ya kuosha mtoto ao kiisha ku badili minyambiyo ya mtoto Kidogo


W.C.
SAVON

**Tunawe mikono yetu mbele ya kula**

**ULIZO1: MUNATAMBUWA NINI KWENYE PICHA HII?**

**JIBU1**: Tuna ona mama nyenye kuosha mikono ya mtoto mbele ya kula. Mama huyo anatumiya sabuni, vyombo viwili, kuna maji safi ndani ya kimoja, Chomba cha pili kinatumiwa ju ya kupokeya maji ya uchafu. Tume ona piya chakula chenye kufunikwa juu ya meza.

**ULIZO 2: SABABU GANI NINAPASHWA OSHA MIKONO YA MTOTO WANGU MBELE YA KULA?.**

**JIBU2**:

- Ju ya kukinga chakula zaidi ya vidudu kutoka kwenye mikono michafu.
- Kama mtoto anakula chakula chenye uchafu, lazima atagonjwa.
- Chakula chenye kuwa na uchafu kinaleta magonjwa ya kuharisha na vidudu vya tumboni kwa watoto wadogo. Kunawa mikono na sabuni ao majivu ina piganisha vidudu vipatikanavyo juu ya ngozi ya mwili. Tuna pashwa ku vizuwiya vi sije kukaa ju ya chakula na kuingiya ndani ya kinwa.

**ULIZO 3: WAKATI GANI TUNAPASHWA KUOSHA MIKONO YA MTOTO?**

**JIBU3**:


- Mbele ya kula
- Kiisha mtoto kutoka kwenye choo3.

**ULIZO 4: NAMNA GANI TUTANAWA MKONO?**

**JIBU4**: Tu napashwa kunawa mikono kwa maji safi na kwa kutumiya sabuni ao majivu

**Habari zingine**

- Nilazima saana mara na mara kuosha mikono ya mtoto, zaidi mbele ya kula, na piya ju watoto wana tabiya ya kutiya vidole vyao ndani ya kinwa.
- Tunapashwa kila mara kunawa mikono mbele ya kutayarisha, na piya mbele ya kipiga chakula


SAVON
SAVON

**Tutumiye kila mara choo safi katika vijiji vyetu**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI KWENYE PICHA HII?**

**JIBU1**: Mtu mumoja anavaa mapapa anaingiya dani ya choo.Tundu la choo liko wazi.

**ULIZO 2: MAHALI GANI INATU PASA KU FANYA CHOO KUBWA?**

**JIBU2**: Ndani la choo ama musarani

**ULIZO 3: TUNALAZIMISHWA NINI WAKATI TU ME TAMBUWA YA KWAMBA MTOTO AME FANYA CHOO KUBWA INJE YA MUSARANI?**

**JIBU3**: Ina tu bidi haraka kutowa mavi yake na ku ya tupa ndani ya tundu la choo.

**ULIZO 4: SABABU GANI TUNA PASHWA KUTOSHA VIZURI MAVI YA MTOTO?**

**JIBU4**: Ju ya kuepusha mtoto asiguse mavi, wala nzii zisije kukaa juu ya mavi na kuambukiza mahali za kandokando.

**ULIZO 5: TUTAFANYA NINI ILI TUSHIKE CHOO ZETU SAFI KILA WAKATI?**

**JIBU5**: Tundu la choo linapashwa kuwa na kifuniko, Nzii zi si kutanane na mavi, mavi haipashwe kuambukiza maji yoyote

**ULIZO 6: MUNA ELEWA NINI JU YA UPATANISHI KATI YA MAVI- NA MAGONJWA YA KUHARISHA KWA WATOTO?**

**JIBU6**: Mangonjwa nyingi, zaidi magonjwa ya kuharisha zinaambukizw kupitiya vidudu vinavyo kuwa ndani ya mavi ya binadamu. Watoto wadogo wanaweza meza hivyo vidudu kama vinapatikana ndani ya maji ya kunwa, juu ya chakula, kwa mikono, ju ya vyombo vya kupigiya chakula ao mahali popote ya kutayarisha chakula nyumabani.

**UKUMBUSHO JU YA NYAKATI KUBWA TULAZAMISHWA KUNAWA MIKONO**

- Kiisha kutoka ndani ya choo,
- Kiisha kupanguza mtoto
- Kiisha kutosha mavi ya mtoto


W.C.

## Tuondowe kila siku uchafu kiwanjani mwetu

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI  KWENYE PICHA HII?**

**JIBU1**: Mtu momoja mwenyi kumwanga uchafu ndani ya tundu ya ngarani, Kiwanja safi popote, choo safi, na pembeni ya nyumba pamejengwa chombo cha mwanzi kwa ajili ya kunawa mikono.


**ULIZO 2: INATU  PASA  KUFANYA NINI  ILI  TUONDOWE VEMA UCHAFU NDANI YA VIWANJA VYETU?**

**JIBU2**: Shika vema majibu na utiye musimamo kwa:

- Uwimizaji kupitiya  muradi wa serikali Muji Safi, ume tupatiya mashauri mbalimbali: tunapashwa ku unguza na kuitupa dani ya tundu ya uchafu ama ngarani. Kwahii mfano wa mwisho, ina tubidi kufinika uchafu dani ya ngarani na udongo ili ya kuepuka  mbuu, panya na vingine vidudu vibaya.

## Habari zingine

Uondowaji wa uchafu ndani ya kiwanja ni lazima juu ya kulinda usafi. Uchafu una wavutiya mbuu,  mende, panya na piya ikisha kujichuya, ina tosha harufu mbaya saana.


W.C.

**Tulinde kila siku upango wetu safi**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI  KWENYE PICHA HII?**

JIBU1: Mama mmoja anamwanga uchafu na masaliyo ya nyumbani ndani ya tundu ya ngarani;

**ULIZO 2: TUNAPASHWA KU FANYA NINI  ILI TUONDOWE UCHAFU YA NYUMBANI  SAWASAWA?**

**JIBU2**: Shika vema na sikiliza majibu:

- Kandokando ya kijiji safi, ni lazima  kuchoma uchafu , na piya kutupa ndani ya tundu ya ngarani uchafu wowote usiwo kuwa tayari kuchomwa. Kwa hii mfano wa mwisho, inafaa kufunika uchafu na udongo kidogo ju ya kuepuka nzii, panya, mende na vidudi vingine.

**Namna ya kutumiya**

Uondowaji wa Uchafu wa nyumbani, ni ya lazima ju ya kukinga usafi,  masalio ya chakula ya nyumabani inavuta nzii, mende na mapanya. Masalio nyingine, kwa mfano vikapo vya kuweka chakula, vina weza patwa na maji ya mvula na kiisha kugeuka makao za mbuu.



**Sisi wote pamoja, tu fanye kazi kwa ajili ya usafi ya mji wetu**

**Namna ya kutumiya**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI KWENYE PICHA HII?**

**JIBU1**: Kiwanja inajaa Majani, Watu wa kijiji moja, wana tumika pomoja, wa baba wamoja wanakata na kuondowa majani kati ya kiwanja chao kwa umiya mipanga, baba mmoja ana fuguwa mufereji na pao ili maji itiririke vizuri, mama mmoja anafagiya kiwanja, na mwengine mama ana towa majani kwa ku tumiya jembe.

**ULIZO 2: INA WEZEKANA WATU WOTE WA KIJIJI CHETU KUTUMIKA PAMOJA?**

**JIBU2**: Sikiliza kwa makini majubu, mafaa ya kazi pamoja ya watu wote kijijini (Ni juu ya kulinda statut ya mji wetu ili ubaki daima safi kila mara, na kupiganisha vidudu vibaya popote)



**Kamati ya Kijiji**

**ULIZO 1: MUNATAMBUWA NINI KWENYE PICHA HII?**

**JIBU1**: Baba Mzee, anakaa mbele ya kundi lenye kuchaganisha vijana, wa mama, wa baba, mganga, na pembeni yawo kunapatikana vyombo vya kusafisha mji (Jembe, Pao, Mpanga, Kifagiyo,

**ULIZO 2: SABABU GANI NI FAIDA KUWA NA KAMATI YA KIJIJI ?**

**JIBU2**: Shika vema majibu na mazungumuzo

**ULIZO 3: KAZI YA KAMATI NDANI YA KIJIJI SAFI NI GANI?**

**JIBU3**: Shika vema majibu na mazungumuzo

